

**Dondoo za mkutano wa Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam
4 Aprili 2009**

Waliohudhuria

Ally Athuman Jumbe
Amos Sindano
Edward Marline
Elia Kimena
Filbert Mbecha
Juma Ali Salehe Jongo
Mejah Mbuya
Mohammed Samwely
Paulo Atibu Hatibu
Selion Elieskia
Shamte J Kigoma
Sosthenes C Amlima

Mradi wa Wamba

Fedha bado hazijafika. Mejah ameonana na wahusika wa NMB (Foreign transfer department) na wakasema wkipata ili document waliyotumia kudeposit hela huko USA ndioy wataweza kushughulika.

Shirika la Fasta Cycle Cooperative

Mejah na Juma walifuatalia wakatapata mihuri kutoka serikali za mitaa lakini serikali ya kata wanasema wanahitaji kwanza barua ya kujitambulisha UWABA. Barua iende kwa katibu mtendeaji wa kata.

Wimbo

Elia alikuja pamoja na Eliasi Kimena na Selemani Anili kuimba wimbo. Tumesikiliza wimbo na amezungumzia vitu muhimu ambavyo wapanda baisikeli vinatukabili. Amesifu mtu aliyetumia bike, haichafui mazingira, ni muhimu kuendesha kwa kufuata sheria, kuvaa helmet na kuwa na taa usiku na kengele nk, wanafunzi na wafanyakazi kuwahi kazini, maombi kwa serikali, husaidia kwa michezo, huondoa msongamano.

Jumamosi ijayo atakuja tena ili kupanga juu ya kwenda kurekodi hiyo single.

Mambo mengine

Paulo alisema tuwe tunasikiliza kupindi cha usalama bora barabarani katika redio TBC saa mbili na nusu.